# Uhalisiamazingaombwe katika Riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika* na *Kufikirika*

*Anna N. Kyamba*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Uhalisiamazingaobwe ni mkondo wa usasa leo. Ni mkondo uliochipuka huko Amerika ya Kusini miaka ya 1960 licha ya kwamba dalili zake zilikuwako kabla katika hekaya na fasihi simulizi za mataifa mengi zikiwemo za fasihi ya Kiafrika na Kiswahili (Mulokozi, 2017). Abrams (1999) anaeleza kuwa nadharia hii ilianza miaka ya 1920 ambayo mwanzoni ilitumika kuhusu wachoraji na baadaye katika bunilizi za kinathari Bunilizi za kinadhari za Jorge Luis Borges (1899-1986) wa Argentina, na halikadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel García Marquez (1927-2014) wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Günter Grass (1927-2015) Mjerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles (1926-2005) wa Uingereza. Kutokana na mawazo hayo ndipo tunapata kujiuliza maswali kuhusu chimbuko la nadharia hii katika fasihi ya Kiswahili ni lipi hasa? Kusema Kezilahabi ni mwasisi wa mkondo huu ni sawa? Ilihali kulikuwa na kazi za Shaaban Robert zenye vimelea vya nadharia hii. Kutokana na mawazo ya wataalamu mbalimbali tunaona kuna haja ya kuchunguza endapo riwaya za Shaaban Robert zina Uhalisiamazingaobwe au la. Katika uchambuzi huu tutajikita katika kuchunguza riwaya mbili ya *Kusadikika* na *Kufikirika*. Riwaya ya *Adili na Nduguze* itatumika pale tu itakapobidi.**

**Maneno Muhimu:** Uhalisiamazingaombwe, *Kusadikika, Kufikirika*, Shaaban Robert

**Utangulizi**

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe, inajulikana pia kama uhalisiaajabu. Bautrice (1985) anadai kwamba uhalisiamazingaombwe inahusishwa na kazi yoyote ambayo inajitenga kwa kiwango fulani na kaida za hali halisi. Kadhalika, Wafula na Njogu wanafafanua kuwa nadharia hii ilichipuka kupinga mihimili ya wanamapokeo ambayo ilikuwa imeegemea katika uhalisia wa mambo, umuundo na mtindo wa kimapokeo (Wafula na Njogu, 2007). Kuasisiwa kwa nadharia ya uhalisiamazingaombwe kunahusishwa na mawazo ya mwanasanaa na mhakiki wa Kijerumani aliyejulikana kama Franz Roh (Zamora, 1995). Ingawa kinadharia inaelezwa kuwa nadharia hii iliasisiwa kunako miaka ya 1920, kiutendaji nadharia hii ilikuwako hata kabla ya muda huo kutokana na sanaa jadia zilizokuwepo kabla ya kipindi hicho. Kama asemavyo Mulokozi (2017) kuwa mkondo huu dalili zake zilikuwapo hata kabla ya miaka ya 1960 katika hekaya za fasihi simulizi za mataifa mengi zikiwemo za Kiswahili. Kutokana na mawazo hayo ndiposa tunaona kuna haja ya kufanya uchunguzi wa riwaya za Shaaban Robert kwa kuzingatia misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe endapo zinaingia katika mkondo huu au la. Uchambuzi wa mawazo ya nadharia hii umefanywa kwa kuzingatia fani na maudhui ya riwaya mbili za mwandishi mashuhuri Shaaban Robert *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1967). Aidha, katika uchambuzi huu tutajikita katika kuangazia vipengele mbalimbali vya muundo, mtindo, wahusika na mandhari. Makala yanaanza kwa kudadisi dhana ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe, mihimili yake, nafasi yake katika uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili. Kabla ya kutoa hitimisho, mjadala wa namna nadharia hii imejitokeza katika kazi husika umefanywa.

Nadharia hii pia ina misingi yake bainifu ambayo inachanganya hali za kimazingaombwe na za kiuhalisia (ukweli). Uchanganyaji huo, unatekelezeka katika misingi ya utunzi na uhakiki wa fasihi. Hii ina maana kuwa kwa kiwango kikubwa misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe haiwezi kutekelezeka nje ya muktadha wa ulimwengu wa kiubunifu. Baadhi ya wahakiki kama vile Abrams (1999) wanadai kwamba dhana na istilahi ya uhalisiamazingaombwe imeanza kunako miaka ya 1920.

Naye Schroeder (2004) anaona kwamba nadharia hii ilibuniwa na kuasisiwa na Mjerumani Franz Roh. Katika lugha ya Kijerumani nadharia hii iliitwa *'Magischer Realismus'* [1]. Hoja kuwa nadharia hii ilibuniwa na Mjerumani aliyeitwa Franz Roh inaungwa mkono pia na Wamitila (2003). Akifafanua zaidi kuhusu nadharia hii, Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa mtu aliyeitwa Franz Roh kutoka Ujerumani aliielezea nadharia ya uhalisiamazingaombwe kwa kirefu katika kitabu chake cha *Nach-expressionismus, magischer Realismus.* Katika andiko hilo inaelezwa kuwa nadharia hii imetokana na hali za uajabu ajabu unatokea katika kazi za kifasihi.

Baadhi ya wahakiki hupenda kuita ujabu ajabu huo unaojitokeza katika kazi za fasihi ni fantasia au umazingaombwe. Ingawa nadharia hii iliasisiwa huko Ujerumani, kutokana na umaarufu wake imeenea na kuathiri mielekeo ya wananadharia wa mataifa mengine kama vile Amerika ya Kusini na hata nchi za Ulimwengu wa Tatu. Bila kujali eneo la kijiografia ambamo nadharia hii imetumika, kwa ujumla wake nadharia ya uhalisiamazingaombwe ni nadharia inayotumika kufasiri miundo na maana ya hali za kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi zinazosawiriwa katika fasihi. Nadharia hii huzichambua hali hizo kwa namna ya moja na kuzifanya zionekane za kawaida (Wamitila, Keshatajwa). Katika nadharia hii, mpaka uliopo kati ya mambo yanayowezekana kuwako na kutokea katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana hutokea katika ulimwengu wa kinjozi, kifasihi na kiuchawi ni mdogo sana.

Naye Abrams (1999:143) anaeleza kuwa istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe', ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na halikadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel García Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Günter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Anaeleza kuwa waandishi hawa wanahusisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalumu katika ruwaza inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya.

Kutokana na ufafanuzi huo tunaweza kusema kuwa uhalisiamazingaombwe ni kuhusisha mambo ambayo hayawezekani katika ulimwengu halisi kupitia utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi na kuyafanya yawezekane na yawe halisi katika ulimwengu usio wa kifasihi (halisi). Maelezo yaliyotajwa hivi punde hayasemi ni wakati gani nadharia hii imechimbuka na kushamiri. Hii inaonekana kuwa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe ilikuwa tangu siku nyingi hata kabla ya kuasisiwa kwa taaluma ya maandishi katika fasihi. Sehemu kubwa ya fasihi simulizi ya Kiafrika Mulokozi (2017) anasema kuwa mtindo huu wa Uhalisia Mazingaobwe unafahamika vizuri kutokana na hadithi za kihekaya na kingano za Kiswahili, kupitia matumizi ya mandhari, wahusika na mitindo ya kufikirika na kinjozi. Kwa upande mwingine wako wanazuoni wanaoona kuwa nadharia hii imechimbuka katika kipindi cha mapinduzi ya viwanda, kipindi cha usasa pamoja na usasa leo (D'Haen 2005). D'Haen (khj: 191) anaeleza kwamba, uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye (postmodernism), linaloonyesha sifa za usasabaadaye kama vile nduni inayojirejelea, yaani uziada uliozidi uhalisia, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuongeza na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi.

Kutokana na kusheheni sifa hizi, kazi zilizoundwa kwa kutumia nadharia hii zimekuwa zikilaumiwa kwa vile humchanganya msomaji kwa makusudi, ili atafakari na avumbue maana zilizofumbatwa na mitindo husika. Mbali na sifa zilizotajwa, kitu kingine kinachoibainisha nadharia hii na ambacho pia huwachanganya wasomaji ni kitendo cha kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti. Kutokana na sifa hii, hata dhana za usasa na ukale hufungamanishwa pamoja. Kwa mujibu wa Khamis (2007) uhalisiamazingaombwe ni aina fulani ya fantasia, na kwa hivyo ni mbinu inayozileta dunia mbili pamoja yaani 'dunia ya ukale' na 'dunia ya usasa'. Kwa pamoja ukale na usasa hujenga misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Katika kazi zilizoundwa kwa kutumia nadharia hii,

[1] Katika kazi yake juu ya mtindo wa sanaa ya kisasa ya Ulaya enzi zile; taz. Roh 1925.

maudhui na fani yana muelekeo wa taathira za kitamaduni, sayansi na teknolojia ambazo zimetokana na mfumo wa kikoloni na baadaye zikaendelezwa hata baada ya ukoloni.

Kwa vile nadharia ya Uhalisiamazingaombwe imehusishwa pia na wazo la usasa na usasa leo, kuna haja ya kufikiria kuhusu usasa wakati wa kufasili istilahi hii. Wafula na Njogu (wameshatajwa) wamejaribu kutuongoza katika hili kwa kutaja na kueleza maana ya jumla ya nadharia za usasa. Kwa mujibu wa wataalamu hawa nadharia za Usasa leo hujumuisha kundi kubwa la nadharia kama vile: Udenguzi, Usemezano na Uhalisiaajabu. Kundi hili la nadharia huonyesha kwamba muwala au mshikamano wa kazi ya kifasihi kama ilivyozoeleka na wanamapokeo si muhimu tena. Hatimaye kutokana na kukosekana kwa muwala huo kazi ya fasihi hujengwa kutokana na mchangamano wa tajiriba zinapatikana ndani ya kazi zinazosomwa na pia zinazopatikana nje ya kazi husika za kifasihi.

Kutokana na maelezo ya wataalamu tuliotaja hivi punde kama vile Danow (1995), Cooper (1998), Zamora (keshatajwa), Encarta Encyclopedia (2002) na Wamitila, (keshatajwa), mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe ambayo ni: Kwanza uhalisiamazingaombwe huwa na matukio ya ajabu ajabu yanayoonekana ya kawaida katika kazi za sanaa ya fasihi. Halikadhalika matukio hayo huwa na hali za kushangaza na kuogofya kwa wasomaji wa kazi husika. Matukio hayo yanakuwa kama mazingaombwe ambayo hustaajabisha. Cooper (keshatajwa) anadai kuwa katika kazi za kifasihi zilizosukwa kiuhalisiamazingaombwe mambo ya kiajabu huelezwa moja kwa moja na kuonekana kama matukio ya kawaida. Waandishi huelezea matukio hayo kwa ufundi kiasi kwamba yanaonekana kama matukio ya kawaida. Wamitila (keshatajwa) anasema kuwa mambo yanayoelezwa ni ya ajabu ama ya kiuchawi ambayo ni sehemu ya mwonoulimwengu wa jamii hizo. Anaendelea kueleza, sababu ya matumizi ya mtindo huu ni kuonesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida yaliyopo katika jamii zetu. Mambo ya ajabu ajabu huweza kusawiriwa kwa namna anuai katika fasihi. Kwa mfano huweza kusawiriwa kama mhusika, mandhari na pia kama msuko ama muundo wa kazi ya kifasihi.

Pili, kazi za kiuhalisiamazingaombwe huchanganya uhalisi na fantasia ama ndoto uhakiki wa kiuhalisiamazingaombwe unamtaka mhakiki ashikilie imani kuwa wakati mtu anapoota ndipo yupo katika uhalisia na wakati yupo katika uhalisia ndipo yumo ndotoni. Malcolm, (1959:94) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala usingizi yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Kutokana na mawazo hayo Wanjiru (2013) naye anaeleza kuwa inaonekana kuwa ndoto zinaendana na mambo mbalimbali yaliyopo katika fikra za mwanadamu. Kazi zilizobuniwa kwa kufuata mkondo huu wa mawazo huwasawiri wahusika wanaoweza kusafiri kifikra au kindoto na kuvuka milima mabonde, nchi kavu, bahari na hata anga. Pia katika kazi hizi, mtu mzima anaweza kurudi katika utoto kimaumbile na kiakili ama kinyume chake.

Tatu, nadharia hii inakiuka mipaka ya utambulisho wa kijamii katika eneo mahsusi la kijografia, kiitikadi na kitaifa. Msingi huu unamaanisha kwa watunzi na wahakiki wa kiuhalisiamazingaombwe wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiwekea uzio ama kujadili mambo katika mazingira finyu kama vile kuegemea mtazamo wa jamii moja, nchi mahususi ama bara moja. Nne, wakati na mahali vina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine au mahali pengine. Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi unaoongozwa na misingi ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe.

Tano, utunzi wa kazi za fasihi unaofuata misingi ya nadharia ya Uhalisiamazingaombwe hufungamana na matumizi ya vipengele anuai vya sanaajadia kama vile visasili na visakale (Abrams na Mulokozi wameshatajwa). Mhimili huu unaelekeza kuwa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe una mwelekeo wa kimwingilianomatini. Tanzu mbalimbali za kisanaajadia kama vile visasili hutumika kuimarisha fani na maudhui ya kazi inayohusika. Katika hatua za utunzi wa namna hii, matukio ya kawaida huwekwa kiukiushi zaidi na kumfanya msomaji atafakari kwa makini zaidi kuliko kama yangeelezwa kwa kutumia mbinu nyinginezo. Jambo hili hufanywa ili kumpeleka msomaji kwenye

safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana pamoja na yasiyowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili ama zaidi.

Mhimili wa sita wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unasisitiza kuwa nadharia hii inapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Yaani kunakuwa na matukio mbalimbali yanayoingiliana na kukamilishana katika utanzu wa fasihi. Hivyo kunakuwa na hali mbalimbali katika kazi za fasihi kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, pia kunakuwa na mwingiliano wa tamaduni za kigeni na asilia. Kutokana na mwingiliano huo kunatokea mkengeuko wa hadhira katika utanzu husika. Kwa ujumla, mihimili ya nadharia ya hii inakiuka kanuni za kiujumi zilizowekwa na wanamapokeo walioandika kazi zao katika karne ya kumi na tisa na ishirini. Nadharia ya uhalisiamazingaombwe inavuka mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa na hatimaye huzalisha fasihi mpya na ya kisasa. Kwa ujumla nadharia hii ina nafasi kubwa katika ulimwengu wa sasa wa fasihi ya kiulimwengu na Kiswahili kwa ujumla.

**Nafasi ya Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe**

Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe ni nadharia ya kisasa ambayo inahusishwa na masuala ibuka ambayo yanatokea katika karne ya ishirini mwishoni na karne ya ishirini na moja. Kazi za kifasihi zinazoegemea katika nadharia hii hujulikana pia kama fasihi za majaribio. Sababu ya kuziita hivyo ni kuwa kazi hizo pamoja na mambo mengine zimeingiza vipengele vya sanaa jadia katika utunzi wake na kuwasilishwa kwa kutumia mitindo ya kifantasia na kimazingaombwe. Kwa hiyo nadharia ya Uhalisiamazingaombwe huziwezesha kazi za fasihi andishi kutumia vipengele anuai vya kifasihi simulizi ama sanaa jadia katika utunzi wake.

Vilevile, nadharia hii ina nafasi kubwa kwa kuwa huifanya hadhira ya wasomaji kuwa makini na kufikiri kwa kina zaidi. Madumulla (2009) anaeleza kuwa kazi za kisanaa zilizojengwa katika nadharia ya Uhalisiamazingaombwe zinafaa pia ziitwe fasihi za kitafakuri. Pendekezo la Madumulla linamaanisha kuwa mkondo wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unasaidia kujenga kazi zinazotafakarisha. Kitendo hiki cha kufikirisha kwa kiwango kikubwa baadhi ya wahakiki wanaona kuwa ndiyo ishara ya ukomavu wa fasihi inayohusika. Katika fasihi ya Kiswahili suala hili limehusishwa mno na kukua na kuendelea kwa utanzu wa riwaya. Kutokana na mawazo hayo tunaweza kusema kuwa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe inakwenda sambamba na wakati na hali halisi ya kijamii. Hivyo matumizi ya nadharia hii hufanya sanaa iende sambamba na maendeleo yanayojitokeza ulimwenguni kote. Kuwepo kwa kazi zinazofuata nadharia hii katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili kunadhihirisha kwamba fasihi ya Kiswahili inakuwa na kubadilika kulingana na maendeleo ya kijamii.

Kwa upande mwingine, licha ya kuwa nadharia hii ni faafu sana katika uhakiki na uchambuzi wa kazi za kisasa katika fasihi, bado utekelezaji wa mihimili yake unakabiliwa na changamoto anuai. Wahakiki wengi wameonya kuwa kila nadharia inafaa tu pale inapofungamana vizuri na kazi ya fasihi, na kwamba kazi moja ya fasihi inaweza kuhakikiwa kwa kutumia mikondo anuai ya kinadharia kutegemeana na haja pamoja na matakwa ya mhakiki. Hali ya uteuzi wa nadharia ya kutumia inategemea malengo ya mhakiki pamoja na ubunifu uliotumika kuunda kazi husika. Kwa kuzingatia usuli huu, nadharia hii hufaa zaidi kutumika kuhakiki kazi za kifasihi zilizoundwa kiajabuajabu ama kimazingaombwe, pia zile zilizo na fantasia. Fasihi hizo bila shaka zitakuwa na matukio ya kifantasia au ya kindoto na kiuchawichawi. Kwa upande mwingine nadharia hii si faafu katika kazi za kisanaa ambazo zinafuata kaida za utunzi wa kimapokeo.

Changamoto nyingine ni kuwa kazi zenye mwelekeo wa kiuhalisiamazingaombwe ni ngumu kueleweka kwa wasomaji. Kutokana na ugumu huo, ujumbe uliokusudiwa na mwandishi au msanii unaweza usifike katika jamii kama alivyotarajia. Kwa mfano riwaya za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za E. Kezilahabi. Ni kazi ambazo zimeegemea katika mkondo wa nadharia hizi. Watu wengi hawazisomi na waliohakiki kazi hizo ni wachache sana kulingana na kutoeleweka kwa kazi hizo. Licha ya dosari hizi za nadharia ya Uhalisiamazingaombwe, endapo mihimili yake itatumika vyema

na kwa tahadhari inaweza kuleta tija kubwa katika utunzi na uhakiki wa fasihi. Katika makala haya tumedadisi ujitokezaji wa mihimili husika kwa kuzingatia riwaya ya *Kusadikika* na *Kufikirika* za Shaaban Robert. Kabla ya uchambuzi wa riwaya hizo tumeanza na kuhoji maoni ya wahakiki mbalimbali kuhusiana na riwaya husika kama ni za kiuhalisiamazingaombwe ama la.

**Je, Riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1967) ni za Kiuhalisiamazingaombwe?**

Riwaya ya *Kusadikika* na *Kufikirika* ni riwaya ambazo ziliandikwa na Shaaban Robert, Riwaya hizi zimechambuliwa na wataalamu mbalimbali kwa kuzingatia nadharia za kimapokeo zaidi. Na wataalamu hao wamezingatia uhakiki wa kazi hizo kwa misingi hiyo kutokana na kipindi kazi hizo zilipoandikwa. Aidha, kuna ukinzani wa mawazo miongoni mwa wahakiki kuhusiana na kazi hizi na uhusiano wake na suala la uhalisiamazingaombwe.

Kuna baadhi ya wataalamu ambao wanaona kuwa kazi za Shaaban Robert kama vile *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguze* zinaingia katika mkondo huu wa nadharia (Walibora 2010). Na wengine wanaona kazi za Shaaban Robert kuna vipengele vinavyohusiana na nadharia hii lakini kazi zenyewe si za kiuhalisiamazingaombwe. Miongoni mwa wahakiki wanaoamini kuwako kwa matumizi ya vipengele vya kiuhalisiamazingaombwe katika kazi za Shaaban Robert ni Khamis (keshatajwa) anayesema kuwa:

> Tunaweza kusema kwamba Shaaban Robert ni mwanzilishi wa riwaya ya fantasia katika fasihi ya Kiswahili, hasa katika *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1952) na *Kufikirika* (1967). Lakini ingawa riwaya hizi zina uhalisia wa aina fulani, fantasia yake ni tofauti na ile ya riwaya mpya, kwa vile zimejikita mno katika ubunifudhaifu wa kila kipengele chake: 'simulizi', 'hadithi', mandhari wa baadhi ya miketo[2] ya matini yake.

Maelezo hayo yanadhihirisha kwamba kwa namna fulani masuala ya kimazingaombwe yalianza kujitokeza katika kazi za Shaaban Robert na kwamba waandishi mbalimbali wameathiriwa na muundo wa Shaaban Robert katika uandishi wa kazi zao. Aidha, Walibora (2010:145) anahoja kuwepo kwa uhalisiamazingaombwe katika riwaya za Shaaban bin Robert kama vile *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1967) kwa kudadisi vipengele anuai vya kifani na kimaudhui vyenye mwelekeo wa kiuhalisimazingaombwe.

Kwa upande wake Wamitila (2003) hafikiri kuwa uhalisiamazingaombwe imeanzishwa na Shaaban Robert, vilevile yeye anaona kuwa suala la upya na usasa katika fasihi ya Kiswahili limezuliwa na Euphrase Kezilahabi. Katika kushadidia hoja yake, Wamitila anarejelea riwaya mpya za Kezilahabi yaani *Nagona* na *Mzingile*. Hata hivyo, Wamitila pia haelekei kukanusha kuwa Shaaban Robert zimesheheni vipengele anuai vya nadharia ya uhalisiamazingaombwe, ingawa anasisitiza mchango wa Kezilahabi katika kuikuza na kuisambaza nadharia hii kupitia utunzi wa riwaya.

Pamoja na kuwako kwa ukinzani wa kimawazo kuhusu asili ya mwelekeo wa kiuhalisiamazingaombwe katika fasihi ya Kiswahili, mtazamo wa makala haya ni kuwa nadharia hii ilikuwepo zamani sana hata kabla ya utunzi wa riwaya ya Kiswahili haujaanza. Vipengele mbalimbali vya nadharia hii zilitumika sana katika uwasilishaji wa sanaajadia mbalimbali kama vile ngano, visaili na vitendawili. Kiuhalisia nadharia mpya na za usasa/usasa leo kama zile zilizobainishwa mwanzoni mwa makala haya zimechimbuka kutokana na mawazo ya nadharia za kale, nadharia za kimapokeo. Kama asemavyo Mulokozi (khj) kuwa mtindo wa nadharia hii unafahamika vizuri kutokana na hadithi za kihekaya na ngano za Kiswahili kama vile *Kusadikika*, *Kufikirika* na *Adili na Nduguye*. Anaongezea kuwa ila katika hadithi hizo msomaji anakuwa anajiandaa kisaikolojia kuyakabili maajabu yanayosimuliwa kwa kuyachukulia kama sehemu ya maisha ulimwengu wa kubuni wa hadithi inayohusika. Anaongezea kuwa katika riwaya za uhalisia mazingaombwe maajabu kama hayo huingizwa katika ulimwengu wa kawaida wa kihalisia.

Nadharia hizo zinachukua mambo yaleyale ya zamani na kuyaweka katika muktadha wa kiusasa ama kiusasa leo ili kusawiri mambo mapya zaidi. Kinachobadilika ni namna ya kuweka msisitizo

[2] Tafsiri ya Chunks

katika kubomoa ama kujenga mtindo mipya ya uwasilishaji wa matukio hayo. Kutokana na maelezo haya kuna uhalisi kudai kuwa kazi za Shaaban Robert kama vile *Kusadikika* na *Kufikirika* zinaweza kuhakikiwa kwa kutumia misingi ama mihimili ya nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Dai hili limetokana na ukweli kuwa ingawa riwaya hizi mbili ziliandikwa zamani sana, maudhui yake ni ya kisasa na mitindo yake imekuwa ikitumika sana katika utunzi wa riwaya za kisasa. Katika makala haya tumechambua riwaya hizi kwa kubainisha jinsi masuala halisi ya kijamii yamesawiriwa kwa kutumia mbinu za kiajabu ama kimazingaombwe. Miongoni mwa mbinu za kimazingaombwe zilizotumika kusawiri masuala nyeti na halisi ya kijamii ni pamoja na mandhari, wahusika, muundo na mtindo wa masimulizi.

**Vipengele vya Kiuhalisiamazingaombwe katika *Kusadikika* na *Kufikirika***

**Mandhari**

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), mandhari hutusaidia kuelewa hisia, imani, tabia maumbile ya wahusika ambayo yanatupa mwelekeo kuhusiana na maudhui. kutokana na fasili hiyo mandhari ni kipengele muhimu cha kifani ambacho hutusaidia kutambua maudhui, wahusika na mwelekeo wa riwaya husika. Katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*, mandhari inayooneshwa na mwandishi ni mandhari ya kufikirika ama ya kidhahania ambayo haipo katika ulimwengu halisi. Kwa namna nyingine tunaweza kusema kuwa mandhari iliyotumika ni ya kimazingaombwe. Aidha, majina ya riwaya zenyewe yanasadifu mandhari ya riwaya husika, kwa mfano katika riwaya *Kusadikika* mandhari yake inaelezwa katika utangulizi wake (na. v) kuwa:

1. Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika kwa mawazo tu. Nchi hiyoipo katikati ya mipaka sita. Kwa upande wa Kusini imepakana na Upepo wa Kaskazini, na kwa upande wa kusini imepakana na Upepo wa Kusi. Mashariki imepakana na Matlai, na Magharibi mpaka wake ni Upepo wa Umande. Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mingine miwili. Mipaka miwili yenyewe ni hii. Kwa juu nchi hiyo imepakana na Mbingu, na kwa chini imepakana na Ardhi.

Kutokana na nukuu hiyo, inajidhihilisha wazi kuwa hakuna nchi ya namna hiyo ambayo ipo hewani na imepakana na nchi hizo zilizobainishwa hapo. Hiyo ni hali ya kimazingaombwe na ni mandhari ambayo ni ya kindoto zaidi. Na mwandishi huyo kaijenga nchi hiyo katika mawazo kama alivyoeleza mwenyewe, hata katika uhalisia huwezi kupata nchi ya namna hiyo katika ulimwengu huu. Anaeleza kuwa nchi hiyo haijawahi kupimwa ili kuiweka nchi hiyo katika ramani, hivyo imekosekana habari za nchi hiyo katika ndoto za wazee. Mwandishi huyu bado anatuonesha kuwa nchi hiyo ipo kwenye fikra na si rahisi kuelezea mandhari yake kwa kuwa haipo kwenye vipimo vya ramani ni ya kufikirika zaidi. Kutokana na hali hiyo anaona kuwa itamsaidia kusimulia simulizi ya hadithi yake kukubalika. Hapa mwandishi anaonesha kwamba aliweka hadithi yake hatika hali ya kimazingaombwe ili kukwepa rungu la serikali ya kikoloni.

Mandhari ya kindoto na kiajabuajabu inajitokeza tena katika safari za wajumbe waliotumwa na nchi ya Kusadikika kwenda kutalii na kuangalia mambo mazuri yanayopelekea maendeleo katika nchi hizo na kuyaandika ili kuleta maendeleo katika nchi ya Kusadikika. Katika safari za wajumbe hao tunaona kuna mandhari za ajabu ajabu zinajitokeza: Kwa mfano mjumbe wa Kasikazini, Kalama anaeleza kuwa alikutana na misitu mikumbwa, nyika za ukiwa na majangwa ya kiu, mito, maziwa na hata bahari uk. 11. Pia kuna mazingira ya mjumbe wa kusini kukamatwa na juju katika nchi ya mfalme jeta ambaye alikuwa ni mfalme wa ajabu ambaye maji yote pamoja na mamilioni ya magogo, chuma, samaki viliingia kinywani mwake uk. 21. Halikadhalika mjumbe wa mbinguni anaelezea mandhari ya Mbinguni kuwa "yalikuwa ya ajabu yaliyosakafiwa kwa yaliyojengwa kwa majohari bora na ya namna ya pekee na dhahabu tupu. Majohari hayo hatakupatikana mahali popote ulimwenguni" Uk. 32. Pia mandhari ya nchi ya Ardhi katika mandhari ya kimazingaombwe. Namna Amini anavyosafiri na kufika katika nchi hizo ni kwa kindoto zaidi. Kwa mfano uk. 42. Karama anasema kuwa:

> Amiri aliona maeneo makubwa ya maji yaliyoitwa bahari, mapana yaliyoitwa maziwa, na marefu yaliyoitwa mito. Rangi na ladha za maji hayo zilikuwa mbalimbali. Kwa kuwa Kusadikika ilikuwa juu ya Ardhi aliyashuku maji hayo kuwa ilikuwa damu ya Wasadikika iliyokuwa ikimwagika kila siku.

Kutokana na nukuu hii, inadhihilisha mandhari ya ajabu ambayo inaogopesha kwa wasomaji. Katika hali halisi huwezi kukuta mandhari ya namna hiyo ya kutisha ambapo hata kwenye maji inaonesha ladha na rangi ya damu. Hivyo tunaona jinsi nchi hizo za jirani zilivyoundwa kwa kimaajabu pamoja na nchi ya Kusadikika yenyewe. Na inadhihilisha kuwa nchi ya Kusadikika ilikuwa ina utawala wa mabavu na kuwakandamiza wananchi. Ndio maana wajumbe walivyoleta habari za maendeleo na namna ya kuikwamua nchi hiyo, walihukumiwa na kudhalilishwa. Licha ya juhudi zao na kujitoa kwao kwa nia ya kuleta maendeleo katika nchi yao. Hivyo mandhari ya kifantasia na kimazingaombwe imetumika katika riwaya ya Kusadikika.

Kwa upande wa riwaya ya *Kufikirika* tunaona mandhari iliyotumika katika riwaya hiyo ni ya mawazoni ama ya kufikirika kama ilivyo katika riwaya ya *Kusadikika*. Halikadhalika mwandishi amechoro mandhari ya nchi ya Kufikirika katika hali ya kidhahania na kifantasia. Kama asemavyo katika utangulizi wa riwaya hiyo:

2. KUFIKIRIKA ni nchi moja kubwa katika nchi za dunia. Kaskazini imepakana na Nchi ya Anasa. Kusini Nchi ya Maajabu, Mashariki Bahari ya Kufaulu na Magharibi Satu ya Milima ya Jitihadi. Ramani ya nchi hiyo vigumu kupatikana kwa sababu nchi yenyewe haiandikiki ila hufikirika kwa mawazo tu. Njia ya kwenda nchi hiyo hukanyagwa kwa fikra sio nyayo. (Uk.vii)

Kutokana na nukuu hiyo, tunaona hali ya mandhari ya riwaya hii ilivyojegwa kindoto au kimazingaombwe. Katika hali halisi hatuwezi kuona wala kukutana na nchi yana namna hii katika hali halisi katika jamii tunazoishi. Katika uumbaji wa madhari hii tunaona jinsi sifa za uhalisiamazingaombwe zinavyojitokeza katika kazi hii. Hata namna ya kufika huko inaonesha huwezi kufika kwa kutumia njia za kawaida bali kifikra. Pia ramani ya nchi hiyo ni ya kufikirika tu wala haiandikiki. Halikadhalika nchi zinazopakana na nchi hiyo ni ya kidhahania ama ya kifikra zaidi. Pia mandhari ya gerezani ambapo inaonekana mjinga na mwelevu wanajadiliana na kuwekeana viapo, katika hali halisi hakuna mazingira ya kujadiliana na kuwekeana viapo gerezani. Mazingira yaliyotumika kuwapata watu wa kafara; kwamba ukulima ulihusishwa na ujinga na biashara kuhusishwa na mtu mwelevu. Vilevile anaelezea mandhari ya nchi ya kufikirika kulikuwa na raha iliyofananishwa na raha ya pepo. Na anaeleza kuwa isipokuwa Kufikirika kuna maradhi na mauti lakini katika pepo uko uzima wa milele. Mandhari ya peponi ni ya kindoto zaidi na inahusiswa na imani za dini za kikoloni kuhusu kuwepo kwa pepo kwa wale wanaotenda mema wangali ulimwenguni. Hakuna mtu hata mmoja aliyeenda peponi na kurudi. Hivyo mazingira ya peponi yapo katika fikra za watu na katika vitabu vitakatifu Biblia na Qurwani hakuna uhalisia katika Pepo anayoisema. Kwa ujumla mandhari aliyoitumia ni ya kidhahania na ni ya kindoto zaidi ambapo ni majawapo ya sifa za uhalisimazingaombwe.

Hivyo katika riwaya hizi mbili tunaona jinsi ambavyo mandhari inavyosawili hali ya kiajabuajabu kama sifa mojawapo ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Kama asemavyo, Mbatiah (2001:60) kuwa, istilahi ya uhalisiajabu inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo, mitindo ya kimazingaombwe inaelezwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Kama tuonavyo katika riwaya hizi kuna mazingira au mandhari iliyotumika ni ya ajabuajabu ambayo hayawezi kupatikana katika ulimwengu halisi.

**Wahusika**

Wahusika ni muhimu katika kazi yoyote ya fasihi kwa sababu ndio wanaopanga mtiririko wa matukio katika simulizi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa wahusika ni nyenzo kuu ya fasihi kwa sababu ndio dira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika. Kama tuonavyo katika riwaya hizi mbili msuko wa matukio pamoja na matendo ya wahusika yamejitokeza katika hali isiyo ya kawaida. Kwa mfano katika riwaya ya *Kusadikika*, mwandishi amewaumba wahusika

wanawake wote katika nchi hiyo huzaa mapacha (uk.v), lakini anaona ni ajabu lakini hakuna mtu aliyewahi kuota wala kusimulia kuhusu matukio hayo ya ajabu. Majina yanaonekana ni ya kawaida lakini yote yanaashiria matendo ya wahusika. Majina kama vile Majivuno, Karama, Bwana Taadabuni, Bwana Komeni, Bwana Fujo, Bwana Boramimi (uk.4) pamoja na majina ya wajumbe kama Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini (uk. 48). Majina hayo yameundwa kulingana na matendo ya wahusika. Majina ya wajumbe pia yanasawiri matendo waliyofanywa ambayo huthaminiwa na viongozi wa nchi.

Vilevile katika riwaya ya *Kusadikika* tunajiuliza maswali mengi kuhusu wajumbe hao ambao walikwenda katika nchi za jirani ambazo mandhari yake ilikuwa ni ya kidhahania. Pia wahusika hao wamejegwa kwa namna ambayo wanakutana na magumu lakini hawakati tamaa. Pia kuna maswali tunayojiuliza kuhusiana na wajumbe hao kwamba; Je walikwendaje katika nchi hizo za jirani, ambazo ramani yake ilikuwa haieleweki? Kwa hali halisi sio kawaida mtu akasafiri kutoka angani kwenda ardhini ama mbinguni na kurudi, mwandishi hajatuonesha ni kwa namna gani wajumbe hao walisafiri. Na tunaona wahusika hao walikuwa wanaondoka wakiwa vijana na kurudi wakiwa wazee. Hii ni ajabu na ni hali ya undoto unaojitokeza. Katika hali halisi haiwezekani, lakini imeezekana kwa sababu matukio ameyajenga kifikra zaidi na mambo mengi kayajenga kindoto. Tukilinganisha na nadharia ya uhalisiamazingaombwe tunaona inajidhihilisha pale ambapo mwandishi anawatumia wahusika kutenda mambo ambayo si ya kawaida katika ulimwengu halisi lakini katika riwaya hii yanaonekana ni mambo yanayowezekana.

Katika riwaya ya *Kusadikika* kuna mhusika malaika katika nchi ya Mbinguni, ambapo tunaona mjumbe aliyekwenda huko anakutana na mhusika malaika ambaye aliyemsaidia kumpeleka mbinguni uk. 32. Karama anasema:

3. Aliandika kuwa kwa msaada wa malaika aliyesimamia mambo ya wanadamu aliweza kufika mpaka katika halmashauri kubwa ya mbinguni. Halimashauri hizo zilikuwa mbili zilizoitwa Hifadhi na Dhahiri.

Mhusika hyo ni wa mawazoni au kidhahania tu na huusishwa zaidi na masuala ya imani, pia hata masuala ya wanawake wazuri na wanaume wazuri ambao wanajidhihilisha kwa matendo yao na wanaimbiwa nyimbo na malaika huko Mbinguni. Wahusika wote hao ni wa mawazoni. Pia tunaona mjumbe wa Ardhini, Amini alivyokwenda huko ardhini ni katika hali ya ajabu ukurasa wa 38 msimulizi anasema kuwa:

4. Wakati wa kwenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku. Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yake yalikuwa majini. Kwa hivi Amini alijifungua, akaogelea bila kuonekana mpaka ufukoni.

Katika hali halisi mtu hawezi kujishikilia kwa ndege na kusafiri hadi chini bila ndege mwenyewe kujua wa binadamu mwenyewe kupata shida. Hii ni hali ya mazingaombwe, ambapo mambo yanatokea hulinganishwa na ndoto ambazo watoto wanaota kama wapo juu wanaruka chini. Hivyo wahusika kama ndege Mandera ambaye aliishi ardhini na kulala Kusadikika, huyo anaonekana ni ndege wa ajabu kweli kuishi nchi nyingine na kulala nchi nyingine. Hali ya malaika na wanadamu kuwasiliana katika ulimwengu halisi haiwezekani.

Kuna wahusika wa kutisha kama Jeta katika riwaya ya *Kusadikika* linalomeza bila kushiba ni mwingilianomatini wa ngano na miviga inayosisitiza kafara katika fasihi simulizi. Mfalme Jeta alikuwa amekaa kitako na kuacha mdomo wazi huku mto mrefu mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa hicho. Kama asemavyo msimulizi:

5. "Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukikwepa kinywa hicho. Tani milioni moja za mwamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji kinywani…lakini kila dakika moja Jeta alilia: Kiu, njaa, kiu, njaa!'…mfalme alitaka kumla Kabuli bila kugawana na wenzake kutokana na uchoyo wake ikatokea vita baina ya majeshi ya mfalme na raia" (uk. 21).

Katika ngano wahusika kama Jeta ni wa kawaida huweza kulinganishwa na mazimwi wanaomeza kila kitu katika fasihi simulizi. Zimwi katika kazi za fasihi simulizi ni mhusika wa kidhahania ambaye anahusishwa na mambo ya kiuchawi na kimazingaombwe zaidi, hivyo mhusika jeta amechorwa katika hali ya kichawi ama kimazingaombwe. Sifa hizo za Jeta zinajitokeza kama mojawapo ya msingi ya nadharia ya Uhalisiamazingaobwe.

Katika riwaya ya *Kufikirika* wahusika wamejegwa katika hali ya mduara mhusika mmoja anajitokeza kwa namna mbalimbali bila wahusika wengine katika riwaya hiyo kumtambua mhusika huyo. Kwa namna nyingine tunaweza kusema kuwa mhusika mmoja ameweza kutumika katika nafasi zaidi ya moja, hali hiyo si ya kawaida katika mtindo wa kimapokeo. Aidha Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa uhalisiamazingaobwe hutumika kusawiri matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) na mambo yasiyowezekana kuwa ya kawaida. Kwa mfano tunamuona Utubusara Ujingahasara ni mhusika ambaye ameshika nafasi tofauti tofauti katika simulizi hilo ama katika riwaya ya *Kufikirika*. Ametumika katika kundi la watabiri, ametumika kama mwalimu na mwisho kama mkulima anayehesabika ni mjinga na anatakiwa kutolewa kafara. Baadaye anatoa ushauri kuwa mtoto wampeleke hospitalini atapona, wanampeleka anapona, wanagundua hayo yote katika ukurasa wa 47. Jina hilo linasadifu mambo yaliyojitokeza katika riwaya hiyo, ambapo kwa hali halisi haiwezekani mtu mmoja kufanya mambo yote hayo pasipo kujulikana.

Majina ya wahusika wengi hayajatajwa, wahusika wengi wamejibainisha kwa majina ya kazi zao kama vile Mfalme, Malkia, Mtoto wa Mfalme, Mkulima, Waziri, Msimamizi, Kadhi na mengineyo. Huu ni muundo wa sanaa jadia. Mulokozi (1996:164) anasema "riwaya za Shaaban Robert zimeathiriwa sana na ngano na hekaya, hasa katika muundo wake na uchoraji wa wahusika wote wakuu ni bapa". Kutokana na mawazo hayo tunaona riwaya hizi zina sifa za uhalisiamazingaobwe kwa kuwa mojawapo ya mihimili ya nadharia hii ni matumizi ya sanaa jadia. Hivyo tunaona matumizi ya sanaa jadia ama vipengele vya fasihi simulizi yametumika katika riwaya hizo.

**Muundo**

Muundo ni msuko ama mpangilio wa visa au matukio katika kazi ya fasihi. Halikadhalika muundo ni jinsi visehemu vyote vya kazi ya kisanaa vinavyohusiana na kuunda kazi nzima ya kisanaa (Mulokozi 1996 na Wamitila 2003). Hivyo muundo hurejelea uhusiano unaokuwepo baina ya vipengele ama visehemu mbalimbali vinavyounda kazi ya sanaa na kuwa kitu kamili. Katika riwaya hizi mbili muundo wake unaelekeana. Muundo ni wa moja kwa moja, visa ni vya ajabu ajabu. Riwaya zote zinahusisha masuala ya sheria na hukumu zisizo za haki pia ni za kiajabuajabu. Usimulizi wa matukio umesukwa kwa ubunifu wa kiwango cha juu. Tukio linaishia na maswali wakati mwingine. Kwa mfano katika riwaya ya *Kusadikika* kisa kinaishia na maswali na hatuoni maswali hayo yakijibiwa; "Nani mwenye haki ya kuyachafua maisha namna hii katika ulimwengu?... Kusadikika itashukuru lini fadhili za watu wake bora?" (uk. 30-31). Pia katika riwaya ya kusadikika hatuoni kama kesi inahairishwa na kusema itaendelea siku inayofuata bali tunaona msimulizi anatuambia siku iliyofuata watu wakazidi kuongezeka. Muundo huu unazua taharuki kwa wasomaji wa riwaya hii.

Vilevile katika riwaya ya *Kufikirika* tunaona muundo wake ni wa moja kwa moja lakini kuna mhusika mmoja amejitokeza mara nne tofauti. Anajitokeza kama mtabili, kama mwalimu, kama mkulima mjinga na ambaye anatakiwa kutolewa kafara na kama mtoa ushauri wa namna ya kumtibu mtoto wa mfalme. Mara zote hizo hawamtambui hadi mwishoni ndio anatambuliwa na mkewe na mtoto wa mfalme. Na inajulikana kuwa wala sio mganga alijiingiza tu kwenye kundi la waganga watabili ili apate kusema aliyoyasema tazama (uk. 47-48). Kwa hali halisi haiwezekani kutokea muundo kama huo wa mtu mmoja kutumika katika sehemu mbalimbali bila kufahamika. Na muundo huo unazua taharuki miongoni mwa wasomaji wa kazi husika. Katika riwaya hizi kmuundo wake licha ya kwamba ni wa moja kwa moja lakini unaibua taharuki na hamu ya kujua nini kinaendelea. Kwa upande wa muundo hausawiri sana muundo wa Uhalisiamazingaombwe kwakuwa muundo wa uhalisiamazingaobwe unakuwa umeparaganyika sana.

**Mtindo**

Mtindo ni ufundi anaotumia msanii kuumba matukio ya kazi ya fasihi. Kwa ujumla mtindo na muundo ni vitu vinavyohusiana. Green (2009) anasisitiza kwamba, mitindo na misingi ya uhalisiamazingaobwe katika fasihi kimatendo ilikuwa ya awali zaidi hasa katika kaida za Kiramsia (Romantism) ambapo masimulizi "yaliweka sambamba matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida". Katika riwaya hizi mwandishi ametumia mtindo wa masimulizi na mwingilianomatini. Katika riwaya ya *Kusadikika* katumia mtindo wa namba mbili na sita, wahusika wa ajabu ajabu kwa mfano mfalme Jeta katika nchi ya Majuju. Pia kuna motifu ya safari na msako ambapo tunaona wajumbe wakisafiri kwenda Kaskazini, Mashariki, Kusini, Magharibi, Mbinguni na Ardhi ilikusaka maarifa. Pia ametumia mtindo wa kidrama na fasihi ya majaribio. Kwa kawaida si rahisi mtu kusafiri kwenda katika sehemu hizo, huu ni muundo wa kimazingaombwe ama kifantasia. Katika *Kufikirika* pia kuna mtindo wa masimulizi, matumizi ya namba moja, mbili, tatu, nne, sita, kumi na sita na thelathini tazama (uk. 32-33 na 48). Halikadhalika kuna matumizi ya waganga wa jadi kwa ajili ya kutibu ugumba wa Mfalme na Malkia. Ambapo makundi ya waganga yaligawanyika mara sita ambayo ni waganga wa mizizi, makafara, mazinguo, hirizi, mashetani na utabiri (uk. 8).

Hivyo katika riwaya hii kuna masuala ya uchawi na ushetani ambapo hii ni sifa mojawapo ya uhalisiamazingaombwe. Msimulizi katika (uk. 11) anasema kuwa kundi la waganga wa mashetani lilikuwa na watu ambao waliweza kuelewa lugha mbalimbali za mashetani. Utabibu wao ulihitaji damu za wanyama, vilemba na pete. Pia masuala ya waganga wa hirizi huusishwa na masuala ya uchawi katika jamii. Kutokana na maelezo hayo inaonesha mtindo wa kishetani na kiuganga pamoja na kiuchawi umetumika katika riwaya ya *Kufikirika*. Pia kuna matumizi ya nyimbo kama mbinu ya fasihi simulizi (uk. 18-19). Wimbo huo unadhihilisha furaha waliyonayo Mfalme na Malkia kwa kupata mtoto. Ni wimbo unaomsifu mtabiri na kuandika jina lake kwa johari zinazongaa ili kila mmoja katika nchi ya Kufikirika amtambue. Haya ni masuala ya kindoto zaidi maana unaweza kuona kwako anafaa kusifiwa na kukumbukwa na jamii nzima wakati ni masuala ya familia na sio masuala ya jamii nzima. Hii inaonyesha uongozi mbaya na ubinafsi ulliokisiri miongoni mwa viongozi wa kisiasa.

Mtindo wa majina ya riwaya zote mbili yanasadifu yaliyomo katika riwaya hizo na majina hayo yanasawiri hali ya uhalisiamazingaombwe. Mfano *Kusadikika*, jina la riwaya hii inaashiria kwamba yale yote yanayoongelewa ama kusimuliwa yanasadikika tu na wala hayana uhalisia. Kwamba mambo hayo yanaweza kuwa ya kweli ama ya uongo, yaani yanahusishwa na masuala ya imani waliyonayo Wasadikika kuhusu nchi yao na sheria pamoja na hukumu zinazotolewa. Hapa mwandishi anawataka wahakiki na wachambuzi waone yanayotendeka na kupinga uongozi mbaya ambao unasababisha unyonyaji, unyanyasaji na ukandamizaji. Pia katika *Kusadikika* walisadiki kuwa "matendo makubwa yoyote yaliamriwa kuanzishwa na kutendwa na watu wenye nasaba bora kama Wafalme na Madiwani" (uk. 3). Hayo ni mawazo ya kitoto ambapo watoto wanaona kuwa wazazi ama walezi wao ndio wanaweza kila kitu. Hata katika (uk. 31) inaonesha Wasadikika wanaona kuwa wao wamepigana vita vingi na wameshinda kumbe wamepigana punde kwa punde na jamii ileile moja yaani yuleyule aliyeshindwa zamani, wakapigana na ndugu yake, mtoto wake na mjukuu wake. Jamii moja inajitokeza kwa namna nyingine yaani jamii moja inajitokeza zaidi ya mara moja bila wao kujua. Hii inafurahisha na kustajabisha kwelikweli, katika hali halisi haiwezekani kutotambua kama unapigana na watu walewale. Hii ni hali ya kindoto na kifantasia zaidi.

Kwa upande wa riwaya ya *Kufikirika* kwa kuangalia jina la riwaya unatambua kuwa riwaya hiyo imejengwa kidhahania zaidi. Na inahitaji wahusika na wasomaji kufikiria mambo mbalimbali kwa njia zinazositahili. Ndio maana tunamuona Utubusara aliposikia mfalme ana haja ya mtoto na anahitaji waganga wa Kufikirika wamsaidie akaona njia mojawapo ya kufahamika ni kwa kujitosa katika kundi la waganga Watabiri ambao wanahitaji utabiri tu na si vinginevyo. Akawa mtabiri na akatabiri kwa namna alivyofikiri. Baadaye ili yatimie yale aliyotabili alijidai kuwa Mwalimu na baadaye kuwa mkulima na baadaye kuwa mshauri wa mfalme na waziri mkuu. Lakini katika hali ya kufikirika zaidi yamefanyika yote hayo, katika ulimwengu halisi haiwezekani kutendeka yote hayo

pasipo kumtambua mtu huyo, hivyo jina la kitabu linakwenda sambamba na mambo mbalimbali yaliyotendeka katika riwaya hiyo. Baada ya uchambuzi huo tuangalie mjada unaonesha kazi teule za Shabaan Robert na miongoni mwa kazi za uhaliamazingaombwe.

**Mjadala**

Kutokana na uhakiki uliofanyika katika kipengele cha tano (5), tumebaini kuwa baadhi ya riwaya za Shaaban Robert zinaingia katika nadharia za Uhalisiamazingaombwe. Riwaya zinazosawiriwa vyema na kuingia katika mkondo wa uhalisiamazingaombwe ni *Kusadikika*, *Adili na Nduguze* na *Kufikirika*. Kuna baadhi ya vipengele vinajitokeza katika kazi hizo ambazo ni sifa mojawapo ya nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Tunadhibitisha kauli ya Walibora (2001) aliposema huenda kazi za Shabani Robert *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1946/1967) ni zina sifa ya Uhalisiamazingaobwe. Aidha licha ya riwaya hizi kuwa na sifa hizo, lakini vipengele hivyo havijidhihilishi waziwazi kama vinavyojitokeza katika kazi za kisasa ambazo zinatungwa kwa kuegemea mkondo huo wa uhalisiamazingaombwe. Kwa sababu katika nadharia za Usasa leo hakuna upya bali huchukua yale yaliyokuwepo na kuyaweka katika mtindo wa kisasa zaidi. Hivyo hata nadharia ya Uhalisiamazingaobwe ilikuwepo tangu wa katika wa Shaaban Robert kwa kiwango kidogo ukilinganisha na hali iliyopo sasa ambayo inatokana na kuongezeka kwa kiwango cha elimu, utandawazi na masuala ya sayansi na tekinolojia.

Muundo na mtindo uliotumika hauoneshi sana mfungamano wa visa, ijapokuwa kwa kiasi fulani unachanganya. Aidha waandishi walioandika kazi kwa kutumia nadharia hiyo kuna muundo wa mkanganyiko zaidi. Yaani katika kazi za uhalisiamazingaombwe muundo wake haueleweki, na hata lugha yake ni ya kisasa zaidi. Kadhalika katika makala haya tunakubalina na Madumulla (2009) anapoeleza kuwa Shaaban Robert ni mmojawapo wa waanzilishi wa riwaya za majaribio. Naye Mulokozi (2017) anaeleza kuwa mabadiliko na majaribio katika bunilizi haukutuwama bali ni mchakato wa kudumu unaoendelea kizazi hadi kizazi. Kwa husema hivi tunatambua kuwa mabadiliko ya utunzi yalianza enzi na enzi na Shaaban Robert ni miongoni mwa watunzi waliojifanya mabadiliko na majaribio katika utunzi wake. Hili linajidhihilisha kwa kuwa mpangilio wa visa na matukio ni wa kifantasia ambayo hayaeleweki vizuri lakini mwisho wa simulizi unaeleweka. Mulokozi (khj) anasema kuwa katika fasihi ya Kiswahili kazi zinazoakisi uhalisiamazingaobwe zimekuwepo hata kabla ya miaka ya 1960, hasa katika hekaya na fasihi simulizi za mataifa mengi ikiwemo fasihi ya Kiswahili. Swali la kujiuliza je kwa nini baadhi ya kazi za Shaaban Robert zina baadhi ya sifa zinazoingia katika nadharia hii na haziweki kama chimbuko la riwaya za mkondo huu? Hasa kwa kuzingatia kuwa nadharia hii imeanzishwa miaka ya 1920 na kazi hizi zimeandikwa baada ya nadharia za usasa kuanzishwa.

Mawazo ya Shaaban Robert katika utangulizi huo anaeleza kuwa sababu ya kukiusha mambo ni kutaka kueleza vizuri yale aliyokusudia. Hii tunaona hata katika ulimwengu wa sasa, waandishi wanafuata mkondo wa nadharia za usasa ili kueleza mambo kama inavyotakiwa. Ijapokuwa uhalisiamazingaombwe umejitokeza zaidi katika kazi za Kezilahabi katika *Nagona* na *Mzingile*. Hata hivyo tunatambua mchango wa Shaaban Robert kama mwasisi wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe kwa sababu aliweza kuonesha mambo yasiyowezekana yaani ya kindoto na kimawazo ameyawasilisha kama mambo ya kawaida na yanayowezekana. Madumulla (1986) anaeleza kuwa alama maarufu iliyoleta athari wakati wa mabadiliko ya fasihi ya Kiswahili ni ile ya Shaaban Robert, baba wa nathari ya kisasa ya Kiswahili, ambaye ametoa mchango mkubwa katika kukuza msamiati wa (lugha ya Kiswahili) na katika sanaa na mtindo wa kuwasilishia kazi za fasihi. Mawazo ya Madumulla ni mojawapo ya udhibitisho kuwa Shaaban Robert ni mmojawapo wa waanzilishi wa riwaya za kisasa kwa kubadilisha mtindo wake wa utunzi. Ambapo alitumia fasihi za majaribio katika utunzi wake na mtindo wa kimwingilianomatini ili kufikisha maudhui yake kwa jamii lengwa. Kutokana na namna hiyo imewapelekea wasomi na waandishi waliofuata (kama vile Kezilahabi, Wamitila na Ahmed Mohamed na Momanyi) kusoma kazi za Shaaban Robert na kuongeza ubunifu zaidi na hasa baada ya kusoma na kuelewa nadharia za Usasa leo.

Kutokana na uhakiki wa riwaya hizo za Shaaban Robert na maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusiana na nadharia ya uhalisiamazingaombwe kuwa ilianza miaka ya 1920. Na wengine wanasema kuwa uhalisiamazingaombwe ni kipengele cha usasa baadaye ambao ulianza baada ya vita vya pili vya dunia kwenda mbele zaidi kuigeuza riwaya ya uhalisia jinsi ilivyokuwa kabla ya kuzuka kwa usasa huko Ulaya (Khamis, keshatajwa). Hivyo ukiangalia mtindo aliotumia Shaaban Robert katika riwaya zake hizo ni wa kifantasia na kimajaribio (sanaa jadia) zaidi. Hivyo inadhihilisha Shaaban Robert ni mwasisi wa sanaa za majaribio katika kazi za riwaya. Pia katika kazi zake ameweza kutumia mandhari ya kidhahania na wahusika wa kidhahania kama mojawapo ya sifa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe vinavyojitokeza kama visasili na visakale.

**Hitimisho**

Kutokana na mjadala huu, Shaaban Robert ndiye mwasisi wa nadharia hii katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu ya uajabuajabu unaojitokeza katika riwaya hizo. Licha ya wataalamu kueleza kuwa Shaban Robert alitumia vipengele vya sanaa jadia kwenye kazi yake na si uhalisia Mazingaombwe (Mulokozi, 2021)[3]. Kutokana na uchunguzi tulioufanya kwenye makala haya na mjadala uliojadiliwa hapo juu ni dhahiri kuwa riwaya hizi zipo katikati ya uhalisi na uhalisiamazingaombwe kwa kuwa muundo wa riwaya zake ni wa kistari. Hivyo basi riwaya za Shabaan Robert zina uhalisiamazingaombwe kwa kiasi fulani kutokana na muktadha husika wa utunzi. Nadharia ya uhalisiamazingaombwe inajitokeza zaidi katika riwaya mpya za kisasa zilizotungwa hasa kwa kuwa waandishi wa riwaya wanatunga kwa kuegemea katika mkondo wa nadharia za Usasa leo. Baadhi ya riwaya hizo ni: *Nagona* (1990), *Mzingile* (1991), *Dunia Yao* (2000), *Bina-Adamu* (2002), *Babu Alipofufuka* (2002), *Nyuso za Mwanamke* (2010) na nyinginezo. Watunzi hawa wanatunga huku wakiegemea katika mkondo wa nadharia hizo kutokana na masuala ibuka yanayotokana na utandawazi na sayansi na tekinolojia pamoja na elimu waliyoipata kuhusu nadharia za kisasa. Mpaka uliopo kati ya uhalisia na umazingaombwe ni mdogo mno kiasi kwamba ni sawa na kwamba haupo katika riwaya hizo. Fantasia na uhalisiamazingaombwe ni mbinu muhimu inayowafanya wasomaji watupie jicho kali katika riwaya mpya (zikiwepo pia riwaya teule za Shabaan Robert) ambazo zimeandikwa kwa kufuata nadharia za usasa leo. Pia zina ukweli wa mambo katika dunia ya sasa, lakini ukweli huo unapatikana katika mkanganyiko wa mawazo na utata kwa wasomaji wa kazi za fasihi husika.

**Marejeleo**

Abrams, M. H. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. Ithaca: Cornell University Press.

Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Literature*: Seeing *with a Third Eye*. New York: Routledge

Danow, K. D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

Encarta Encyclopaedia (2002). *New York*. Microsoft Company Limited.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S.A.M. (2007). "Utandawizi au Utandawazi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai". Massamba, D.P.B. (2007) (Mhr). *Jarida la Kiswahili.* uk . 49-64 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. TUKI.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishirs Limited.

Malcolm, N. (1959). *Dreaming U.S.A*. London. Routledge and Kegan Paul Ltd.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics & Publishers.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao.* Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Oxford University Press.

Mulokozi, M. M. (1996). Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: OUT.

[3] Katika kumbukumbu ya Euphrase Kezilahabi mwaka 2021.

Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Robert, S. (1967). *Kufikirika*. Nairobi: OUP.

Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Roh, F. (1925). *Nach-Expressionismus – Magischer Realismus. Probleme der neuesten europäischen Malerei.* Leipzig: Klinkhardt & Biermann.

Schroeder, S. (2004). *Rediscovering Magical Realism in the Americas*. Westport: Praeger.

Wafula, R.M. na Njogu. K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2010). "Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*". *Swahili Forum* 17(2010): 143-157.

Wamitila, K.W. (1991). "*Nagona* and *Mzingile:* Kezilahabi's Metaphysics". Kiswahili 60: 62-67.

Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia na Uhalisiaajabu katika Riwaya Mpya: Babu Alipofufuka (Said Ahmed Mohamed) na Watu wa Gehenna (Tom Olali). Idara ya Isimu na Lugha Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Zamora P. L. na Faris, B. W. (1995). *Margical Realism: Theory, History and Community.* London. Duke University Press.